# UHAKIKA WA CHAKULA HUONDOA UMASIKINI (IDUO)

Mfuko wa maendeleo ya jamii (TASAF III) kwa utekelezaji wa awamu ya kwanza unaondelea kufanyika nchini kote umeonyesha mafanikio makubwa katika juhudi za kunusuru kaya masikini. Mafanikio hayo yameonekana kuleta tija kwa walengwa na yamejipapazua bayana pale timu ya wataalam wa Kitengo cha TASAF Kongwa ilipofanya ziara kupata picha halisi ya namna ambavyo walengwa wameweza kunufaika na kuinua hali zao za kimaisha kama ilivyothibitishwa na Mkazi wa kijiji cha Iduo, Kata ya Iduo, Wilaya ya Kongwa, ***Anderson Andrea Kusalula*** mlengwa mwenye umri wa miaka 56 (010301010104842).

***Mlengwa huyo alipohojiwa kuhusu mafanikio aliyoyapata toka aanze kupokea ruzuku ya kunusuru kaya maskini alisema, hadi sasa amepokea awamu 22 tangu mpango wa kunusuru kaya masikini uanze kutekelezwa Wilaya ya Kongwa, Yeye hupokea ruzuku ya Tshs. 44,000 kila baada ya miezi miwili (2), ambapo Tshs. 20,000 ni ruzuku ya msingi, Tshs. 8,000 ni ruzuku ya ziada, Tshs. 8,000 ni ruzuku ya mtoto mmoja anayehudhulia kliniki na Tshs. 8,000 ni ruzuku ya watoto wanao soma shule ya msingi.***

**HISTORIA YAKE KABLA YA MPANGO**

***Bwana Kusaluta*** aliendelea kuieleza timu historia ya maisha yake kabla ya kuingia kwenye mpango wa TASAF na alisema, hali ya maisha yake kabla ya kuanza kupokea ruzuku ilikuwa ngumu sana iliyopopelekea kushindwa kuwatimizia watoto wake mahitaji muhimu ikiwemo kuwapeleka shule. Alisema kuwa kaya yake ina jumla ya watu tisa (9), watoto wawili (2) waliochini ya miaka mitano (5) wanao hudhuria kliniki, na watoto wawili (2) wanasoma shule ya msingi. Kusalula alisema ***"Hali ya kipato changu ilikuwa chini sana kwa sababu familia yangu ilikuwa kubwa na hali ya njaa hivyo si kumudu kulima eneo kubwa japo tuna mashamba ya ukoo. Muda mwingi nilikuwa nahangika kutafuta chakula kwa kulima vibarua kwa wenzangu.***

**BAADA YA KUINGIA KWENYE MPANGO**

Alipoulizwa namna alivyonufaika na ruzuku ya kunusuru kaya maskini Bwana Kusaluta alisema, baada ya kupata fedha za ruzuku alizitumia kununua nguruwe mmoja (1), aliyemfuga hadi alipokuwa mkubwa na kuamua kumuuza kisha kununua nguruwe wawili (2) ambao nao pia aliwauza na kupata fedha za kununulia nguruwe wanne (4). Badaye anasema aliwauza wote wanne (4) na kupata Tshs. 800,000/=, kati ya hizo alichukua kiasi cha Tshs. 600,000/= akanunua

mabati 35 na Tshs. 200,000/= aliwekeza kwenye kilimo cha mtama, ambapo alipata chakula cha kutosha, hivyo ruzuku yake ikawa anaitumia kununulia mbao, nondo na nyingine kumsaidia katika shughuli zake za shamba.

***"Kabla ya mpango nilikuwa naishi kwenye nyumba ndogo sana, kama unavyo iona" Bwana Kusalula alisema aliamua kufayatua matofali ya kuchoma kwa sababu udongo na upatikanaji wa magogo kwa ajili ya uchomaji wa matofali hayo ni rahisi pale kijijini.***



**MAFANIKIO ALIYOPATA**
***Na Sopi Samwel***

"Mzee Anderson amefanikiwa kujenga nyumba ya matofali ya kuchoma iliyoezekwa kwa jumla ya mabati 35. Kuhusu kilimo amelima ekari 8 alizochanganya mtama pamoja na karanga, pia ana shamba la mahindi ekari 4. Lakini pia nina ekari zingine 4 za Mahindi"

Alipotakiwa kueleza amewezaje kumudu kulima ekari nyingi namna hiyo, Bwana Kusaluta alikuwa na haya ya kusema “hili shamba ni la ukoo na kabla ya kuingia kwenye mpango wa kunusuru kaya maskini nilikuwa siwezi kulima. Hivyo mara tu nilipoingia nilianza kukodisha wakulima wa kutumia jembe la kukokotwa na ng’ombe. Kipaumbele changu kikubwa nilipenda kuanza kulima zao la mtama, hii ni kwa sababu linavumila hali ya ukame, hivyo nilianza kupata mavuno na baadae niliuza na hela ninayopata niliitumia kwa mahitaji mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuweka watu wa kunisaidia shughuli za kilimo”. Aliendelea kueleza kuwa “ukitaka kushinda umasikini kuwa na uhakika wa chakula ni lazima kufanya kazi na kuweka akiba ya kili tunachokipata baada ya kuuza sehemu ya mazao tuliyopata.”



*Nyumba Mpya ya Bwana Anderson aliyoijenga baada ya kunufaika na fedha za mpango wa TASAF III wa kunusuru kaya maskini.*

**MASHUUDA WA KUSALULA**

**Shuhuda wa kwanza**: - Jirani yake bwana Anderson, ndugu Jeska Mwijumbe anasema "Mzee ***Kasalula amejitahidi na alikuwa anaishi kwenye kajumba kidogo sana lakini sasa amefanikiwa kujenga nyumba kubwa".***

**Shuhuda wa Pili**:- Kaimu Mtendaji wa Kijiji cha Iduo ndugu Nicolus Richard ***anamwelezea Kusalula kuwa ni mmoja wa walengwa waliofanya mambo makubwa, " angalia anashinda shambani ni mchapa kazi huyu mzee"***

Mwanakamati wa mpango wa kunusuru kaya masikini Bwana Thobias alimweleza Mzee Anderson kuwa maono yake ni makubwa na kuwa utambuzi wake ni wa kweli kwamba upo wakati mpango wa kunusuru kaya maskini utafikia ukomo wake. Hivyo ni vema kutumia vizuri ruzuku hii



*Bwana Anderson akionesha eneo la shamba alilolima mtama na mazao mengine.*

**MFUKO WA MAANDELEO YA JAMII WAWAPAISHA KIELIMU WALENGWA**

Mwanafunzi Sifael Charles Kusenha miaka 19 mhitimu wa kidato cha nne shule ya vipaji maalum ya Kilakala Sekondari iliyopo mkoani Morogoro ni miongoni mwa wanafunzi walionufaika na ruzuku ya masharti ya elimu katika Wilaya ya Kongwa. Famila ya Sifael ni wakazi wa kijiji cha Mbande Wilaya ya Kongwa.

Familia hiyo hupokea kiasi cha Tshs. 44,000 kila baada ya miezi miwili (2) hii ikiwa ni pamoja na ruzuku ya elimu ya msingi Tshs. 10,000 kwa kuwa ina watengemezi wenye umri chini ya miaka 18, mwanafunzi mmoja (1) wa Sekondari na mwanafunzi mmoja (1) wa shule ya msingi.

**KWA NINI SIFAEL**

Historia ya binti huyu toka familia yake ilipoingia kwenye mpango wa maendeleo ya jamii (TASAF) 2014, mpango huo ulitoa nuru kwa kuwa kabla ya mpango huo binti huyo alikuwa akipata shida sana hata kupata mahitaji yake ya msingi alipokuwa shuleni ilikuwa ni kwa taabu. Sifael alisema ***"nakumbuka kabla ya mpango huu hali yangu ilikuwa ngumu sana kwani kuna kipindi hadi walimu pale shuleni na wanafunzi wenzangu walikuwa wakinisaidia, hata nauli ya kurudi nyumbani"***.

Aliendelea kueleza kuwa mpango wa TASAF III, wa kunusuru kaya masikini kulitoa matumaini mapya kwani mama yake Bi. Anjelina Kusenha, alipoanza kumtumia matumizi kila alipokuwa akipokea ruzuku. "Matumaini yangu yalianza kuzinduka niliposikia familia yangu imeingizwa kwenye mpango wa kunusuru kaya masini, kwani niliona mama akijinyima kunitumia matumizi japo hali ya pale nyumbani ilikuwa mbaya, mama aliona umuhimu wangu kusoma" alisema Sifael kwa hisia.

Mafanikio kitaalum na matokeo ya Sifael yamezivutia familia nyingi masikini baada ya matokeo yake ya kidato cha nne 2017 kuibuka na ufaulu wa daraja la pili alama 19 katika mtihani wake wa kidato cha nne.



*Sifael Charles kusenha akiwa shuleni Kilakala*

**TASAF IMEMSAIDIAJE?**

Alisema kuwa alipoanza kuwa na uhakika wakupata mahitaji yake alianza kujiona kama na yeye ni binadamu kama walivyo wengine, faraja yake ilirudi na kujikuta akichukia umasikini na kuanza kusoma kwa bidii. Alisema kwa hisia za ndani ***"Pesa ya ruzuku kutoka TASAF zimenisaidia sana niliichukulia kama motisha ya kusoma ili niisaidie familia yangu iondokane na umasikini ilionao".***

Anjelina Charles Kusenhani, mama yake na Sifael akielezea alivyo msomesha binti yake kwa shida alisema ***" kila nilipo pata ruzuku yangu nilimtumia mtoto wangu kidogo kwa ajili ya matumizi hata kama kwa serikali imefuta ada lakini bado mahitaji ya mtoto wa kike ni ya lazima hivyo ilikuwa kila ninavyopata ruzuku namtumia"***.

Sifael anatoa shukrani kwa Serikali na Uongozi wa TASAF, aliomba mpango huu uendelee kumsaidia atakapo ingia kidato cha tano mwezi wa tano mwaka huu. Naye Mratibu wa Mpango wa TASAF wa kunusuru kaya maskini ***Bw.Unambwe Erasto*** alimhakikishia kuwa TASAF itaendelea kufuatilia maendeleo yake ya kitaaluma na itamuunganisha na shule yoyote ya Serikali ndani ya Tanzania atakayokuwa amepangiwa. Mratibu huyo alimsisitiza binti huyo kutoa taarifa zake katika ofisi ya Mtendaji wa Serikali ya Kijiji atakapokuwa amepangiwa shule ili TASAF waweze kumuunganisha kwenye mfumo wa masharti maana TASAF inatoa ruzuku ya masharti hadi mwanafunzi wa kidato cha sita.

Mtendaji wa kijiji cha Mbande **Bw. Hasasan Janga** naye alisema ***" Familia ya Kusenha inaishi katika mzingira magumu sana, ila huyo binti ana historia ndefu , kwanza hata shule ya msingi alisoma kwa kuunga unga, kumbe alikuwa na kipaji alipofanya mtihani wa darasa la saba alifaulu na kupangiwa shule ya vipaji maalum"***.

Kwa upande wake Afisa Maendeleo ya Kata ya Sejeli Bi Mercy Mchovu pamoja na Mwanakamati wa malipo ya TASAF bwana Mawazo Kilatu walisema Sifael ameonyesha kuwa umasikini si kigezo cha kushindwa kusoma.



*Sifael Charles kusenha akiwa Nyumbani kwao Mbande*

## MALENGO NA NIDHAMU YA MATUMIZI YA FEDHA YAKOMBOA KAYA MASKINI MBANDE

Vumilia Manyelezi John miaka 75 ni mnufaika wa mpango wa maendeleo ya jamii TASAF Wilaya ya Kongwa, Kata ya Sejeli, Kijiji cha Mbande ni mmoja wa wanufaika 151 wanaopokea ruzuku ya mpango wa kunusuru kaya masikini.

Kaya ya Hidaya ni moja kati ya kaya 151 ambazo zinapokea ruzuku ya Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini unaoendeshwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii TASAF.

Bi. John anapokea Tshs 20,000/= kila baada ya miezi miwili ikiwa ni ruzuku ya msingi ya Tshs. 10,000/= kwa kuwa hana mtengemezi mwenye umri chini ya miaka 18 wala mwanakaya anaye hudhuria kliniki au shule. Historia ya mama huyu toka alivyoingia kwenye Mpango wa

maendeleo ya jamii (TASAF) ni ya mfano kwa jamii na walengwa wengine. Kipindi anatambuliwa kuwa kaya maskini alikidhi vigezo vyote vya kaya maskini na aliishi kwenye nyumba mbovu naya tembe iliyoezekwa kwa matope, mlo wake kwa kutwa ulikuwa mmoja tena mara nyingine kwa kubahatisha kutokana na ukame wa mara kwa mara.

Bibi huyo alisema "***nyumba niliyoishi wakati huo kama unavyoiona na ni ya miaka mingi iliyopita"*** Bi Vumilia anaonyesha kijumba cha tembe kidogo huku akitabasamu na kuongeza kuwa TASAF imenikomboa sana. Huku akitabasamu, aliendelea kusema "***Wajukuu zangu isingekuwa TASAF leo hii ninge kuwa bado naishi kwenye hiki kijumba cha tembe***".

Alipo ulizwa kwa sasa kama haitumii hiyo nyumba ya tembe au anaitumia, Bi Vumilia alimshika mkono mwandishi wa habari hii na kusema "***angalia hii nyumba mjukuu wangu***. ***Pembeni ya nyumba ya tembe kulikuwa na nyumba ya udongo iliyoezekwa kwa bati ya vyumba vitatu ambayo alijenga alipoanza tu kupata ruzuku mwaka 2015".***



***Bi Vumilia Manyelezi John akiwa na mjukuu wake***

“Awamu ya kwanza na ya pili nilipoanza kupokea ruzuku niliona hela ndogo sana kwa sababu wenzagu niliona wakipata hela nyingi, niliumia sana moyo kwa sababu sikujua kwa nini mimi Napata fedha kidogo wakati wengine naona bado vijana wanapata hela nyingi kuliko mimi”. Anasimulia mama huyo kwa hisia na kuongeza kuwa “siku moja nikiwa kwenye kituo cha malipo alikuja mwezeshaji mmoja simkumbuki jina alikuwa mdada mnene maji ya kunde kabla ya malipo alitoa semina naona ilinitoa tongotongo.

Mama huyo ambaye ana umri mkubwa lakini anakumbukumbu alisema mwezeshaji wa siku hiyo alimpa maono makubwa maana alisema fedha hizo ni sawa na mbegu inatumika kidogo lakini siku ya mavuno utavuna kiasi kikubwa. Akinukuu mama huyo alisema mdada huyo alisema “hii muichukulie kama mbegu, kwani mnapoenda shamba kupanda mbegu ekari moja huwa mnakwenda na mbegu kiasi gani watu wote waliitika debe moja, akauliza tena je, huwa mnavuna kiasi gani, wote tukaatikia gunia 10” tangu siku hiyo nilianza kununua mabati moja kila malipo.

Mwezeshaji wa kijiji cha Mbande bwana Mawazo Kialatu na Bi. Rehema Chaheka wa kitogoji cha Kisimani wanasema huyu bibi ni wamfano kati ya walengwa anapata hela ndogo sana lakini anafanya vizuri sana. Maneno yao yalisapotiwa na Bi. Rusy Malejehe Tip mlengwa wa TASAF katika hicho kitongoji Kijiji cha mbande. Mjukuu wa Bi Vumilia Bw Baraka Manyerezi alisema bibi yangu huwa hazibomoi nyumba zake anaziacha tu ili uwe ukumbusho kama mnavyoona hapa hili tembe watoto wake wote kawazalia kwenye tembe, amejenga nyumba nyingine ambayo tunaitumia kwa sasa lakini kama unavyoona kuna hii nyumba nyingine ya tofali za bloku hapa”.



Nyumba iliyojengwa na Bi Vumilia Manyelezi John  baada kuanza kupokea ruzuku

Mwandishi wa habari hii alijionea nyumba ndogo ya bloku ambayo ujenzi wake umekaribia kufika mwishoni iliyoezekwa mabati yenye chumba kimoja na sebule. Kutokana na kutokuwa na kipato kikubwa nyumba ameamua kujenga nyumba ndogo ili aweze kumuda gharama za ujenzi ambazo anasema ziko juu sana. Nyumba hii sasa itanitofautisha na wenzangu ambao wanapokea lakini hawajui namna ya kuzitumia vema fedha za ruzuku, aliseama bibi huyo.



*Nyumba mpya iliyojengwa Bi Vumilia Manyelezi John*

Mama huyu alikuwa na mipango thabiti ya kujikomboa kutokana na ruzuku aliyopokea na haoni tabu kusema yaliyo moyoni mwake. Anasema kwa maisha aliyoishi hapo awali mambo yalikuwa hayendi. Ilifika wakati alikata tamaa na kujiona kuwa ataishi maisha duni siku zote. Malipo ya Tshs. 20,000/= anazopokea kila baada ya miezi miwili (2) ambazo pia zina mahitaji mengine ameweza kujenga vyumba hivi.

Bi Vumilia “Kila ninapopewa ruzuku yangu kiasi shilingi elfu kumi naitumia kwa mahitaji ya kuwekeza kwenye maduka ya vifaa vya ujenzi ili kuboresha makazi yangu . Inayobaki ni kwa ajili ya chakula” Anaeleza Bi Vumilia

Alianza kununua bati moja moja kila malipo yanapofanyika alijiwekea utaratibu wa kurudi na bati moja hatimae leo amefanikisha kujenga nyumba ya chumba kimoja ya kudumu. Fedha alizojengea hazikutoka kwenye vyanzo vingine bali ni ruzuku pekee ya TASAF. Pamoja na kuwa anapokea ruzuku ya TASAF, Bi. Vumilia ni mkulima wa mahindi na mtama. Anasema kuwa mwaka huu amelima ekari moja ya mtama na ekari 2 za mahindi.

Msimu wa mwaka jana 2017 hakuweza kupata mazao ya kulima katika shamba lake kutokana na mvua kidogo. Pamoja na ukame uliotawala kwa kipindi kirefu, shamba lake la mtama limestawi vizuri japo shamba la mahindi limeathiliwa na jua hivyo kutegemea mavuno kiasi kidogo.

Bi Vumiali anayo shauku ya kuanzisha shughuli za ufugaji wa kuku na mbuzi lakini changamoto aliyonayo ni nguvu kazi ya kuhudumia kwani yeye anaishi na mjukuu wake mmoja tu. Ruzuku anayopata anasema imemsaidia vya kutosha na anatoa shukrani kwa TASAF na Serikali kwa kumweka kwenye Mpango na anasema hakuwaangusha kwani ametumia fursa aliyoipata kujikwamua kutoka kwenye hali mbaya ya maisha.

Bi Vumilia anamalizia kwa kutoa ushauri kwa wenzake ambao wanaendelea kupata ruzuku kupitia mpango wa kunusuru kaya maskini. “Natoa wito kwa wenzangu nao watumie vizuri fedha hizi, usije mpango ukafika mwisho wakaachwa na umasikini zaidi; Wafuate ushauri tunaopewa na wanakamati kuhusu matumizi mazuri ya fedha na wasisahau kuweka akiba na kuanzisha miradi ya ujasiriamali kwani hiyo ndiyo njia pekee ya kuweza kujikwamua”

## KUTOKA BANDA LA NGURUWE HADI KUJENGA NYUMBA

Mkazi wa kijiji cha Mtanana "B", Bi Merry Stanley Sepeku mwenye umri wa miaka 44 ni mnufaika wa Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini unaoendeshwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii TASAF. Sepeku hupokea kiasi cha Tshs. 36,000/= kila baada ya miezi miwili (2) ikiwa ni ruzuku ya msingi Tshs. 20,000/=, ruzuku ya malipo ya ziada Tshs. 8000/=, ruzuku ya wanafunzi wawili (2) wa shule ya msingi Tshs. 8000/=.

## MAISHA KABLA KUWEKWA KWENYE MPANGO WA TASAF

Kabla ya kuingia kwenye mpango wa kunusuru masiki TASAF, maisha ya Sepeku yalikuwa magumu sana kwani aliishi kwenye mabanda ya nguruwe yaliyojengwa na kikundi cha wakina mama. Pia hali ya chakula haikuwa nzuri kwa kuwa hakuweza hata kujishughulisha na kilimo badala yake muda mwingi alifanya kibarua kwa ajili ya kujitafutia hela ya kununua chakula kwa ajili ya watoto wake. Bi Merry alisema "***Nilikuwa sina hata shamba, muda wangu mwingi, niliutumia kufanya vibarua kwenye mashamba ya watu"***. Bi. Sepeku anasimulia kwa uchungu na akaendelea kusema kwamba ***"thamani ya utu wangu kwa jamii haikuwepo kabisa nilionekana mtu wa ajabu ajabu tu"***.

## MAISHA BAADA YA MPANGO

Bi. Sepeku alianza safari ya kujikwamua kimaisha mwezi Septemba, 2014, baada ya malipo ya awamu ya kwanza na awamu ya pili alipokea mwezi Septemba pia awamu ya tatu anakumbuka alipokea mwezi Januari 2015. "Mikupuo hiyo mitatu ya malipo ilibadilisha maisha yangu kabisa, nilijitahidi kutunza hizo fedha na kuwekeza kwenye kilimo cha alizeti. Haikuwa kitu rahisi kufanya uwekezaji huo, anasimulia Bi Sepeku huku anatikisa kichwa kukumbuka hali ya ufukara aliyokuwa nayo wakati huo.

Akisimulia nyumbani kwake Bi Sepeku anasema baada ya kupata ruzuku yake aliienda kwa mama yake mkubwa aliyepo hapo hapo kijijini na kuomba shamba ili aweze kuanza kulima, mama yake mkubwa alimpa shamba ekari tatu, alipanda alizeti. Alifanikiwa kuvuna gunia 10 ambazo aliuza na kupata Tsh 530,000/=.

Bi. Sepeku anasimulia kwa tabasamu akasema "mwaka 2015 maisha yangu yalianza kubadilika maana nilipata eneo nikaanza kujenga nyumba, nilitumia Tshs. 250,000 kwa ajili ya fundi na gharama za kufyatua tofali, wakati huo nilinunua bati 8 nikaezeka".

Baada ya kuezeka nilihamia kuanza kuishi mimi, watoto wangu na mdogo wangu na kutoyaamini macho yangu na maisha yangu ya awali niliyokuwa nalala kwenye banda la kufugia nguruwe. Bi. Sepeku aliendelea na kilimo na kuongeza kununua bati hadi sasa ana bati 24.



*Bi Sepeku akiwa mbele ya nyumba aliyoijenga kupitia ruzuku aliyoipata.*

MAFANIKIO BAADA KUINGIA KWENYE MPANGO

Bi.Sepeku amefanikiwa kujenga nyumba iliyoezekwa bati 24, kufanya biashara ndogondogo kipindi cha kiangazi ikiwemo kuuza mbogamboga kutoka Kibaigwa. Amenunua "Solar" ,kujenga choo cha kisasa na kuwanunulia watoto wake mahitaji ya shule ikiwemo sare za shule. "ndugu mwandishi hapa kama unavyo niona hiki kibanda changu nimekiwekea nishati ya umeme jua (solar energy) unaotusaidia kupata mwanga nyakati za usiku pamoja na matumizi mengine kama kuchaji simu na wanafunzi kujisomea nyakati za usiku.



*Bi. Sepeku akiwa mbele ya choo cha kisasa alichokijenga kupitia ruzuku aliyopokea.*

Mjumbe wa Serikali ya Kijiji cha Mtanana "B", Bw. Noel alipomzungumzia Bi. Sepeku Gupa alisema "***Bi. Sepeku namfahamu tangu akiwa anaishi kwenye banda la nguruwe alilopewa na wasamalia wema, hali yake wakati huo ilikuwa ngumu sana, leo hii amekuwa mfano hapa kijijini kwetu".***

Alipotakiwa kutoa ushauri kwa walengwa wenzake Bi. Sepeku alisema ***“kila fedha unayoipata lazima uiwekee malengo kwa kuwa hakuna fedha ndogo au nyingi, kinachotakiwa ni kujiwekea malengo tu hiyo ndo siri ya mafanikio”.*** Aliishukuru Serikali kwa kuanzisha mpango huu kwani yeye umemsaidia. Alihitimisha kwa kusema ***“ Usingekuwa mpango huu sijui leo hii maisha yangu yangekuwa vipi”.***

## BI HAGU NA MANUFAA ALIYOYAPATA KUPITIA MPANGO WA KUNUSURU KAYA MASKINI.

Bi. Hagu Kornelio Mlugu miaka 65 ni mkazi wa kijiji cha Mlanga, Kata ya Kongwa Wilaya ya Kongwa. Bibi huyu ni mmoja kati ya wanufaika 221 wa Mpango wa TASAF kunusuru kaya masikini. Kaya ya Bi. Mlugu ina wanafunzi 3 wanaosoma shule ya msingi na wanafamilia wengine wa 4. Bi Hagu hupokea ruzuku ya Tshs. 40,000/= kila baada ya miezi miwili (2).

Akizungumzia manufaa ya mpango wa kunusuru kaya maskini Bi. Hagu anaelezea hali ya maisha yake kwa sasa yamepiga hatua, kwani alikuwa akiishi maisha ya shida sana. Upatikanaji wa chakula ulikuwa washida sana, mahudhurio ya watoto shuleni yalikuwa hafifu na kwa upande wa makazi anasema alikuwa akiishi nyumba ya tembe lililoezekwa na majani nikiwa na watoto wa tano na ndugu wengine.

Hangu anasema nyumba ya tembe ndiyo aliyoishi miaka yote, aliingizwa kwenye mpango wa kunusuru kaya masikini TASAF mwaka 2014. “***Nilipoanza kulipwa fedha hizo, sikufanya masihara, nilianza kwa kununua kitoto cha nguruwe kimoja baada ya malipo ya kwanza kwa Tshs. 10,000”,*** alisema.

Anasema, ukubwa wa famila ulimfanya ashindwe kufanya shughuli nyingi za kujiongezea kipato kwa sababu muda mwingi alifanya vibarua kwa watu ili apate fedha kwa ajili ya chakula. Baada ya kuingizwa kwenye mpango aliweza kujishughulisha na kilimo na kuanza kupata mafanikio makubwa.

Bi. Hagu aliendelea kusema “nikamuuza ***nguruwe wa kwanza na fedha zilizopatikana nililima ekari 3, baadae nilivuna alizeti hizo magunia 10, baada ya mauzo ya alizeti nilinunua ng’ombe mmoja kwa kiasi cha Tshs. 120,000/= na mabati 11 kwa kiasi cha Tshs 110,000/=”***. Anaongeza kwa kusema “***kwa sasa pamoja na hayo yote niliyoeleza nafunga na kuku wapatao 10 na bata 12 ili waweze kuniongezea kipato pale ninapokuwa na mahitaji ya haraka”*** .

Alipotakiwa kuonyesha mafanikio mengine, Bi. Hagu alisema ana ng’ombe wawili ambapo anatarajia kununua tena wengine kama mavuno ya mwaka huu yatakuwa mazuri.



“Nimelima ekari 2 za alizeti pamoja na karanga, ekari 2 za mtama kama hali ya mvua itaenda vizuri nina uhakika wa kuongeza ng’ombe mwingine na kuendelea kuboresha makazi yangu” alisema Bi. Hagu kwa tabasumu

Bi. Hagu alisema anashukuru TASAF na Serikali kuanzisha mpango huu kwani umeinua kipato na kumtoa kwenye dimbwi la umasikini. “Naishukuru serikali kuniingiza kwenye mpango wa kunusuru kaya masikini, nawahasa wenzangu watumie vizuri pesa wanazopata, wasitumie kunywa pombe bali wazitumie kuwekeza kwenye maendeleo”.